

RITA YAKUSUDIA KUZIFUTA TAASISI 300 AMBAZO HAZIJATEKELEZA AGIZO LA KUHUISHA TAARIFA ZAO

HABARI NA PICHA ZA MATUKIO

Tarehe 21 Octoba 2016

Wito umetolewa kwa Bodi za Wadhamini wa Taasisi na Asasi za Kiraia kote Nchini kuhakikisha zinajitokeza na kuwasilisha taarifa za Taasisi zao kabla ya mwisho wa mwezi Oktoba mwaka 2016 kwani RITA bado inaendelea na zoezi la kufuta taasisi/asasi zote zilizoshindwa kuhuisha taarifa zake.

Akizungumza na Waandishi wa habari hii leo Jijini Dar es salaam Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi Emmy K. Hudson amesema kuwa tayari Taasisi 181 zimeshafutiwa usajili wa bodi za wadhamini baada ya kujiridhisha katika hatua ya awali ya uhakiki na nyingine 300 ziko mbioni kufutwa katika daftari la Msajili Mkuu iwapo zitashindwa kuwasilisha taarifa zao.

Bi Hudson ameongeza kuwa Asasi nyingi za kiraia zimekuwa na malengo mazuri ya kuisaidia Serikali katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii pindi zinapoanzishwa na kusajiliwa lakini inafikia wakati mwingine hubadili malengo yaliyokusudiwa na kuzitumia taasisi hizo kwa kujinufai-sha binafsi na hata kufikia hatua ya migo-goro isiyokwisha na kuhatarisha amani na usalama.

“Zipo taasisi ambazo zinaanzishwa kwa kipindi fulani kwa mfano kuna mfadhili ameahidi kusaidia kifedha lakini pesa zikishaingia tu ndipo kutoelewana huanza na baadaye kufikia hatua mbaya ya ubadhirifu wa mali za taasisi husika na kufikia kuzitelekeza bila ya uongozi.”

Ikumbukwe kuwa mwezi Aprili mwaka huu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria Dkt Harrison Mwakyembe aliagiza RITA kusitisha usajili mpya wa Taasisi za kijamii na badala yake kufanya uhakiki ili kuchambua Taasisi ambazo ni mfu na zile zisizofuata sheria na taratibu za kuanzishwa kwake.

Taarifa kwa vyombo vya Habari



Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Bi Emmy Hudson akizungumza na Waandishi wa Habari katika ukumbi wa mikutano wa RITA Makao Makuu Jijini Dar es salaam kuhusu kusudio la kuzifuta Bodi za Wadhamini wa Taasisi zote ambazo hazijawasilisha taarifa zao kwa ajili ya uhakiki katika zoezi linaloendelea kwa Asasi za Kijamii, Vyama vya siasa, Michezo na Taasisi za Kidini.